**TAARIFA YA MAENDELEO YA MTOTO INAYOSOMWA NA MKURUGENZI MTENDAJI (W) BIBI CHANGWA MKWAZU KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA INAYOFANYIKA KIJIJI CHA MBUYUNI KATA YA MBUYUNI TAREHE 16.06.2017**

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kijiji
Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM (W),
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri (W),
Mkurugenzi Mtendaji(W)
Waheshimiwa Madiwani,
Katibu Tawala (W),
Wakuu wa Idara
Afisa Tarafa.
Mtendaji wa Kata, watoto wote,
Walimu wote,
Wananchi wote mabibi na mabwana.
Asalaam aleikhum,
Bwana Yesu Asifiwe,
Habari za asubuhi.

**Watoto oyeeeee!!**

**1.0. UTANGULIZI**

Mhe. Mgeni rasmi,
Leo tupo kwa ajili ya kumsherehea mtoto wetu, ni siku ya mtoto wa Afrika.
Mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane (18) (kulingana na mkataba wa umoja wa Mataifa juu ya haki ya mtoto na sheria ya mtoto ya Tanzania 2009). Siku ya mtoto wa Afrika huadhimishwa kila mwaka kwa lengo la kukumbuka mauaji ya watoto zaidi ya 600 waliouwawa katika kitongoji cha Soweto nchini Afrika Kusini mwaka 1976. kutokana na kuandamana kupinga sera za makaburu za kubadili mfumo wa elimu kwa watoto wa Afrika. Siku hii ilipitishwa na umoja wa Afrika kwa azimio namba 51 la mwaka 1990, na ilianza kuadhimishwa rasmi mwaka 1991, na kuanzia wakati huo siku ya Mtoto wa Afrika imeendelea kuadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 16 Juni katika nchi zote zilizo wanachama wa umoja wa Afrika.

## 2.0.UTEKELELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA WATOTO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI.

Katika kutekeleza kwa vitendo ujumbe wa siku ya mtoto wa Afrika tarehe 16.06.2017 ambao ni "***Maendeleo Endelevu 2030 Imarisha Ulinzi na Fursa Sawa kwa Watoto"*** Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kadiri ya mpango wa maendeleo ya Wilaya.Masuala ya msingi yaliyotekelezwa yalilenga kuleta ustawi wa mtoto ikiwa ni pamoja na :-

- Kutoa msaada kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.
- Kuboresha huduma ya afya kwa watoto na wajawazito.
- Kuendeleza elimu kwa wanafunzi walio ndani ya shule na nje ya shule.
- Kushughulikia masuala yote ya ukatili na unyanyasaji wa Watoto kupitia kitengo cha ustawi wa jamii.

## 2.1. KUTOA MSAADA KWA WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA HATARISHI.

Mhe. Mgeni rasmi,
katika Halmashauri ya Wilaya Masasi wapo watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na pia wapo wenye kuishi na virusi vya UKIMWI (VVU). Takwimu zilizopo kwa mwaka 2016/2017 watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ni 196 na watoto 285 wanaishi na VVU, kati yao wavulana ni 124 na wasichana ni 161. Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imeendelea kuwasaidia watoto walio katika mazingira hatarishi, ambapo katika bajeti ya 2016/2017 imetenga jumla ya Tsh **7,984,000**/= kwa ajili ya kuwasaida watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kupata huduma muhimu za shule kama vile kalamu,sare,madaftari. Ambapo kwa mwaka 2016/2017 sare za shule zitatolewa kwa wanafunzi 100, viatu jozi 100,daftari 15 kwa kila mmoja kwa wanafunzi 100 na kalamu boksi 31.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kupitia idara ya Afya imefanikiwa kuwapatia sare za shule,kalamu kwa watoto 150 zenye thamani ya **Tsh 2,250,000/=,** na kuwakatia kadi za Afya ya Jamii (CHF) zenye thamani ya **Tsh 250,000**/= Lengo ni kuwasidia watoto hao waweze kupata mahitaji yao ya msingi,hivyo natoa wito kwa jamii kuwasidia watoto walio katika mazingira

hatarishi ili waweze kupata mahitaji yao ya msingi. Lakini kutoa taarifa sahihi za watoto wa jinsi hiyo.

## 2.2. KUBORESHA HUDUMA YA AFYA KWA WATOTO NA WAJAWAZITO.

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imeendelea kuhakikisha huduma ya Afya zinaboreshwa ili kuhakikisha mtoto anapata haki ya kuishi, kulindwa, na kufurahi. Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imefanikiwa kutoa chanjo zifuatazo kwa watoto:

- Chanjo ya Vitamini “A” kwa watoto 3742 walio chini ya miaka (5) kati ya watoto 2449 waliotarajiwa sawa na asilimia 152
- Pia Hamashauri imetoa chanjo ya kuzuia kifua kikuu (BCG) kwa watoto 3548 kati ya watoto 2449 waliotarajiwa sawa na asilimia 144
- Chanjo ya polio kwa watoto 3361 kati ya watoto 2449 waliotarajiwa kupata chanjo hiyo sawa na asilimia 137
- Vile vile Hamashauri ya Wilaya ya Masasi imefanikiwa kutoa chanjo ya kuzuia kifaduro, donda koo, homa ya ini na tetenasi kwa watoto 3396 kati ya watoto 2449 waliotarajiwa sawa na asilimia 138
- Pia imetoa chanjo ya sulua kwa watoto 3742 kati ya watoto 2449 waliotarajiwa sawa na asilimia 152

Pamoja na mafanikio haya bado wapo wazazi ambao hawajapeleka watoto wao kupata chanjo hizo hivyo naomba wazazi/walezi na jamii kwa ujumla kushiriki na kuwapeleka watoto kupata chanjo mbalimbali zinazotolewa na serikali ili kuwakinga watoto wasipate maradhi yanayotokana na ukosefu wa chanjo hizo.

Ndugu mgeni rasmi, Halmasahuari ya Wilaya ya Masasi kupitia kitengo cha Ustawi wa Jamii imefanikiwa kushughuikia matatizo mbalimbali ya watoto yahusuyo ukatili na unyanyasaji wa watoto ambapo imefanikiwa kutatua na kutoa ushauri wa kisaikolojia kwa watoto wapatao thelathini na mbili (32). Lakini Halmashauri imefanikiwa kutoa msaada wa kisheria kwa watoto kumi na moja (11).

Lengo la kutoa msaada huo ni kumlinda mtoto dhidi ya ukatili na unyanyasaji unaofanywa na jamii dhidi ya watoto, ili kuimarisha ulinzi na furaha sawa kwa watoto kama kauli mbiu ya mtoto wa Afrika mwaka 2017 inavyosema "***Maendeleo Endelevu 2030 Imarisha Ulinzi na Fursa Sawa kwa Watoto".***

Ndugu Mgeni rasmi kuendeleza watoto walio mashuleni na nje ya shule,
Halmashuri ya Wilaya ya Masasi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanikiwa kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuendeleza mtoto aliyopo ndani na nje ya shule juhudi ambayo imezaa matunda kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imefanikiwa kusajili wanafunzi 10,851 wa darasa la kwanza (wavulana 5577 na wasichana 5274). Wanafunzi waliofanikiwa kufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2016/2017 walikuwa ni 1751 kati yao Wavulana 853 na Wasichana 898, walioripoti shuleni walikuwa wanafunzi 1562 (Wavulana 757 na Wasichana 805 )sawa na asilimia 89, wanafunzi waliobadilishiwa shule walikuwa 47 (Wavulana 23 na wasichana 24) sawa na asilimia 3 na wanafunzi 62 walikwenda shule za Watu binafsi miongoni mwao (Wavulana 32 na Wasichana 30). Wanafunzi 80 hawakuripoti shuleni kati yao Wavulana 41 na Wasichana 39 sawa na asilimia 5. Lakini pia Halmashauri ya Wilaya inaendelea na programu ya MEMKWA kwa watoto waliokosa elimu ya darasani. Kutokana na changamoto ya baadhi ya wanafunzi kutohudhuria masomo nachukua fursa hii kuwahimiza wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni.

Kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi napenda kuyashukuru mashirika yasiyo ya kiserikali (NG'OS na CBO's), Waheshimiwa Madiwani,Viongozi wa Kata na wadau wengine waliowezesha Halmashauri ya Wilaya Masasi kufikia mafanikio hayo na bado tunaendelea kuwaomba tuendeleze ushirikiano wetu ili kuwafanya watoto wetu wapate ulinzi na furaha sawa na hatimae Tanzania ipate maendeleo endelevu. Lakini watoto wakwepeni hao mafataki kwa tamaa ya fedha au vinginevyo.

***"MAENDELEO ENDELEVU 2030 IMARISHA ULINZI NA FURSA SAWA KWA WATOTO" 16/06/2017.***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**